

## **MKATABA WA UPANGAJI**

Mkataba huu umefanyika kati ya **Ndugu Asnath .O. Mollel wa S.L.P 8000**, Arusha, Mwenye nyumba, iliyopo eneo la Sakina, Kata ya Elarai, Manispaa ya Arusha. Ambaye atatajwa kama ni **“MWENYE NYUMBA (YARD)”** katika mkataba huu.

Na

**Zekwa Trading Company Limited wa S.L.P 16460**, Arusha. Ambao nao watatajwa kama ni **“MPANGAJI”** katika mkataba huu, nayo makubaliano ni kama ifuatavyo:-

1. Mwenye Nyumba amekubali kumpangisha Mpangaji vyumba viwili, pamoja na Eneo lake lenye ukubwa wa **Sqm 3593**, kwa ajili ya kufanyia biashara, kwa kipindi cha Miaka Kumi, kuanzia **tarehe 01/03/2021** hadi kuishia **tarehe 28/2/20231** na endapo Mpangaji atapendelea kuongeza kipindi kingine cha upangaji wake. Nae Mwenye Nyumba asipokuwa na sababu za kumkatalia, utafanyika Mkataba mwingine kufuatana na majadiliano na maafikiano ya wakati huo.
2. Kodi ya upangaji huu ni **Tshs 500,000/=(Laki Tano Tu)**, kwa mwezi mmoja, kodi ambayo italipwa mara moja kila baada ya miezi kumi na mbili yaani kila mwaka mmoja mmoja **Tshs 6,000,000/=(Millioni Sita Tu)**. Nae Mwenye Nyumba kwa kuiweka saini yake katika Mkataba huu anathibitisha makubaliano ya kupokea jumla ya **Tshs 6,000,000/=** toka kwa Mpangaji zikiwa ni kodi ya upangaji kwa kila mwaka.
3. Mpangaji haruhusiwi kuipangisha nyumba au eneo hilo kwa Mpangaji mwingine Zaidi yake, wala haruhusiwi kuvifanyia aina yoyote ya marekebisho kabla ya kupata idhini toka kwa Mwenye Nyumba kwanza.
4. Mpangaji atawajibika kujilipia matumizi yake ya umeme na maji kikamilifu bila kulimbikiza madeni. Na malipo hayo ni mbali na kodi ya upangaji huu.
5. Mpangaji atawajibika kuitunza nyumba hivo katika hali ya usafi pamoja na mazingira mengine, na siku ya kuhama atawajibika kuikabidhi kwa Mwenye Nyumba ikiwa katika hali yake waliyokabidhiwa nayo hapo mwanzoni.
6. Mpangaji akiukatiza upangaji wake yeye mwenyewe, hawatakuwa na haki ya kumdai Mwenye Nyumba amfidie kwa kipindi ambacho atakuwa amekwisha kukilipia na bado kutumika, labla iwe ni Mwenye Nyumba ndiye aliyeukatiza.
7. Mpangaji atawajibika kuomba kwa Mwenye Nyumba kipindi kingine cha upangaji huu mwaka mmoja, kabla ya Mkataba huu kufikia mwisho wake, nae endepo atakubaliwa awe tayari kuingia Mkataba Mpya na kulipia kipindi kingine mara tu kitakapoanza.

Mkataba huu tumeandikiana hapa mjini Arusha, Tumeusoma, Tumeuwelewa na kukubali ya kwamba ni sawa kwa kuziweka saini zetu tukiwa na akili timamu bila ya kulazimishwa wala kushawishiwa leo tarehe 25/2/2021.


Saini yangu Mimi Mwenye Nyumba

  
.....  
MRS. ASNATH O. MOLLEL.

Saini ya shahidi wa Mwenye Nyumba

*O. mollel*  
.....  
MR. OLAIRIVAN MOLLEL


Saini ya upande wa Upangaji


  
.....  
MR. ZEPHANIA S. KWAYU (M.D)  
ZEKWA TRADING CO.LTD

Saini ya shahidi wa Wapangaji

*Ru.*  
.....  
MRS. RACHEL .Z. KWAYU

Saini ya Mwandishi wa Mkataba huu

*ALEX ANTHONY KAYA*  
  
.....  
Commissioner for Oaths

  
ALEX ANTHONY KAYA  
Advocate,  
Notary Public  
&  
Commissioner  
for Oaths  
P.O. Box 39456, DAR ES SALAAM